**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

Anwani ya Simu: "ELIMU" Simu: 026 296 35 33
Baruapepe: info@moe.go.tz
Tovuti: www.moe.go.tz

Mji wa Serikali - Mtumba,
Mtaa wa Afya,
S.L.P 10,
**40479 DODOMA**

Unapojibu tafadhali taja:

**Kumb. Na. GA.80/145/01A/57**

**21 Novemba, 2024.**

Mwenyekiti,
TAMONGSCO,
S.L.P. 2662,
**DODOMA.**

Katibu Mtendaji,
Christian Social Services Commission (CSSC),
S.L.P. 1454,
**DAR ES SAALAM.**

Katibu Mtendaji,
Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA),
S.L.P. 21422,
**DAR ES SAALAM.**

Mwenyekiti,
Tanzania Association of Private Inventors in Education (TAPIE),
S.L.P. 13346,
**DAR ES SAALAM.**

Mwenyekiti,
Baraza la Sunnah Tanzania (BASUTA),
S.L.P. 8581,
**DAR ES SAALAM.**

Mkurugenzi,
Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET),
S.L.P. 13547,
**DAR ES SALAAM.**

Mwenyekiti,
TAWOSCO,
S.L.P. 2458,
**DODOMA.**

Umoja wa Wazazi Jumuia ya CCM,
S.L.P.3,
**DODOMA.**

## WARAKA WA ELIMU NA. 03 WA MWAKA 2024 KUHUSU KALENDA YA MIHULA YA MASOMO KWA SHULE ZA AWALI, MSINGI NA SEKONDARI MWAKA 2025

Tafadhali rejea kichwa cha habari.

2. Kwa kuzingatia umuhimu wa kuwa na idadi sahihi ya siku za masomo, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeandaa **Kalenda ya Mihula ya Masomo kwa Shule za Awali, Msingi na Sekondari kwa mwaka wa masomo 2025**.

3. Ni muhimu kuzingatia utekelezaji wa Kalenda husika kwa ufanisi ili kuepuka changamoto ya kutokamilisha ufundishaji na ujifunzaji wa mada zote kwa wakati na hivyo kulazimika kuweka mipango ya ufundishaji na ujifunzaji inayowanyima watoto/wanafunzi fursa ya kupumzika na kushiriki kikamilifu katika shughuli za kijamii katika familia na jamii zao.

4. Kalenda ya Mihula ya Masomo kwa Shule za Awali, Msingi na Sekondari kwa mwaka 2025 ni kama ifuatavyo:

| MIHULA | KUFUNGUA MUHULA | LIKIZO FUPI | | KUFUNGA MUHULA | IDADI YA SIKU ZA MASOMO |
|---|---|---|---|---|---|
| | | KUFUNGA | KUFUNGUA | | |
| Muhula I | 13/01/2025 | 11/04/2025 | 22/04/2025 | 06/06/2025 | 98 |
| Muhula II | 08/07/2025 | 29/08/2025 | 15/09/2025 | 05/12/2025 | 96 |
| **Jumla ya Siku za Masomo** | | | | | **194** |

**Tanbihi:**

- Siku za Masomo kwa mwaka ni **194**.
- Mashindano ya UMITASHUMTA yatafanyika tarehe 08/06/2025 hadi 21/06/2025, na UMISSETA yatafanyika tarehe 22/06/2025 hadi 04/07/2025.
- Mashindano ya Michezo ya Shule za Sekondari za Afrika Mashariki (FEASSSA) yatafanyika tarehe 17/08/2025 hadi 29/08/2025.
- Ili kupunguza muda mwingi wa mapumziko kwa wanafunzi ambao unaweza kuathiri ratiba za masomo, na kwa kuzingatia kuwa mwaka ujao ni mwaka wa uchaguzi, Kamishna wa Elimu amelazimika kufanya maboresho katika Kalenda ya Mihula ya Masomo kwa mwaka 2025 kama ilivyokuwa imewasilishwa awali.

5. Kutokana na maboresho hayo, Waraka huu unafuta Waraka Na. 02 wa Mwaka 2024 uliotolewa na kusambazwa wenye **Kumb. Na. GA.80/145/01A/56** wa tarehe 8 Novemba, 2024.

6. Nawatakia utekelezaji mwema.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
**KAMISHNA WA ELIMU**

**Nakala:** Wathibiti Wakuu Ubora wa Shule Kanda na Wilaya,
**TANZANIA BARA.**

**Katibu Mtendaji**, Baraza la Mitihani la Tanzania.

**Serikali za Mitaa, Sauti ya Wananchi,**

**Jitokeze Kushiriki Uchaguzi**